UTATHMINI WA UMILISI

GREDI YA 4

MUHULA WA KWANZA 2024

SHUGHULI ZA KISWAHILI

JINA: _____TAREHE_____

SHULE: _____

1. ***Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1- 5***

   (Dani na Jeni wamekutana njiani Jeni alipokuwa akielekea dukani) Dani: Haya

   mwenzangu, habari za utokako? Naona una haraka kwelikweli.

   Jeni: Oh! Umenishtua sana. Sikuwa nimekuona. Habari nzuri tu ... naam nina haraka kidogo maana mama amenituma maziwa ya kuwatayarishia wageni wake chai. (*Anajipangusa uso*)

   Dani: Samahani. Naomba dakika moja tu unieleze jambo. Wajua jana sikuja shuleni. Nilikuwa nikisokotwa na tumbo. Je, mwalimu wa Kiswahili alipeana kazi gani ya ziada?

   Jeni: Oh, pole. Natumai umepona sasa. Bi Tausi alipeana kazi mradi ya kutayarisha makasha ya nomino, vitenzi na vivumishi kisha kuandika mifano na kuitia humo. Ni rahisi tu. (*Akitabasamu)*

   Dani: Ahaa! Ni rahisi kweli. Nitakwenda sasa hivi kuianza kazi hiyo.

   Jeni: *(Akiondoka kwenda*) Sawa Dani?

   Dani: Sawa kabisa. Nashukuru kwa maelezo yako. Ni

   kwa nini Jeni alikuwa na haraka?

   A. Alitaka afike dukani haraka anunue alichotumwa.
   B. Hakutaka kuongea na Dani
   C. Alitaka afikishe alichotumwa nyumbani.
   D. Alitaka kuanza kazimradi waliyoagizwa na mwalimu.

2. Jeni alikuwa akienda dukani kununua nini?

   A. Sukari
   B. Majanichai
   C. Mkate
   D. Maziwa

3. Jeni alishtuka kwa sababu

   A. Dani aliongea kwa sauti ya kutisha.
   B. hakuwa amemwona Dani.
   C. mama yake alitaka arudi nyumbani haraka.
   D. alikuwa amekawia bila kumwona Dani.

4. Kazimradi waliyoagizwa kuifanya ilihusu haya yote ila?

   A. nomino.
   B. vitenzi.
   C. vielezi.
   D. vivumishi.